

Mbinu, Dhima na Athari za Kumuanika Nje Mfiwa katika Utendaji wa Utani wa Wahehe

*Asifwe Mwagike na Edith B. Lyimo
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

Ikisiri

Utani ni kipera cha mazungumzo/nyambi katika fasihi simulizi chenye dhima mbalimbali kwa jamii husika. Lengo la makala hii ni kuchunguza mbinu, dhima na athari za kumuanika nje mfiwa katika utendaji wa utani wa Wahehe. Maswali tunayojobu ni: Je, ni utani upi unaojitokeza wakati wa kumuanika nje mfiwa? Nini dhima na athari ya utendaji huo wa utani kupitia mbinu ya kumuanika nje mfiwa? Data za utafiti huu zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya mahojiano na ushuhudiaji wa misiba na kuchambuliwa kwa kutumia Nadharia ya Utendaji na Uamilifu. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa mbinu ya kumuanika nje mfiwa pindi anapopatwa na msiba hufuata hatua kadhaa wakati wa utendaji wa utani. Utendaji wa utani huo kupitia mbinu ya kumuanika nje mfiwa huwa na dhima kama vile; kudumisha umoja na ushirikiano, kupunguza majonzi kwa wafiwa, kuilinda amali hii muhimu ya utani mionganoni mwa wanajamii, kuonya na kuburudisha. Makala hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu; utangulizi, kiini na hitimisho. Utangulizi unaeleza kwa ujumla dhana ya utani pamoja na nadharia zilizotumika. Kiini kinaelezea mbinu, dhima na athari za kumuanika nje mfiwa katika utendaji wa utani wa Wahehe. Sehemu hii imefuatiwa na mbinu za kiutendaji wa utani wakati wa kumuanika nje mfiwa, dhima, athari zake na mwisho hitimisho.

Maneno Muhimu: Utani, Utendaji, Kuanika, Mfiwa, Dhima, Athari.

Utangulizi

Neno utani linatokana na kitenzi ‘tania’ ambacho kina maana ya kumfanyia mtu dhihaka, stihiza, mzaha au masihara bila ya kukusudia kumkera (King’ei na Kisovi 2005). Wataalamu hawa wanaendelea kufafanua kuwa utani ni kiungo cha mila na desturi katika jamii. Aidha, katika fasihi utani hupatikana katika utanzu wa mazungumzo/nyambi (Mulokozi 1996). Utani hujitokeza kwa namna tofautifofauti katika miktadha tofauti kutegemea na uhusiano uliopo baina ya mtu na mtu, jamii na jamii na hata kabilan na kabilan. Msingi mkuu wa desturi hii ya utani ambayo ilikuwepo tangu jadi mionganoni mwa makabila mengi ni kujenga uhusiano mwema na kuondoa mbali uhasama na chuki. Pia, utani huweza kutumika kwa lengo la kuleta ucheshi kwa njia ya kumuumbua mtu kwa kumkejeli na kumrudi mtu ye yeyote ambaye ana tabia mbaya ili afuate maadili ya kijamii. Lengo la makala hii ni kujadili mbinu, dhima na athari za kumuanika nje mfiwa katika utendaji wa utani wa Wahehe.

Data za makala hii zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji na mahojiano. Katika mbinu ya ushuhudiaji matukio kadhaa ya misiba katika jamii ya Wahehe likiwemo la kumuanika nje mfiwa yалиshuhudiwa. Aidha, njia ya mahojiano ilitumika kuwahoji watoa taarifa wanne (4) juu ya mbinu zinazotumika kumuanika nje mfiwa dhima pamoja na athari zake. Data za utafiti huu zilikusanywa kati ya mwezi Oktoba na Desemba 2021.

Uchambuzi wa data hizi umefanyika kwa kutumia Nadharia ya Utendaji na Nadharia ya Uamilifu. Nadharia ya utendaji ni matokeo ya mawazo ya wataalamu wa fasihi, anthropolojia, ethnoisimu na sosholojia (Fine 1994 na Bauman 2011, 2012). Schechner (2013), anafafanua mihimili ya Nadharia ya Utendaji kama uwepo wa fanani na hadhira, muundo wa kiutendaji pamoja na uwepo wa mawasiliano kulingana na tamaduni za jamii husika. Baadhi ya vipengele vinavyopaswa kuzingatiwa wakati wa utendaji ni pamoja na kiimbo, miyondoko, mapigo, toni, uigizaji na mbinu za utendaji. Makala hii imechambua data kwa kutumia Nadharia ya Utendaji ili kufafanua mbinu zinazotumika kumuanika

nje mfiwa katika utendaji wa utani wa Wahehe. Kimsingi katika Nadharia ya Utendaji, fanani ndiye mtendaji mkuu akisaidiana na hadhira kufinyanya kazi ya fasihi katika utendaji wake kupitia mambo kama vile; kupiga makofii, kuruka na kuimba. Hivyo, pande hizo mbili haziwezi kutenganishwa katika suala la utendaji, kwani utendakazi wa fanani hutegemea hadhira ili kutoa mwitiko fulani. Kwa hiyo, kutokana na umuhimu wa utendaji wa utani katika jamii ya Wahehe Nadharia ya Utendaji imetusaidia kujuu mbinu zinazotumika kumuanika nje mfiwa wakati wa utendaji wa utani.

Nadharia ya Uamilifu iliasisiwa na wanasosholojia Auguste Comte, Herbert Spencer Vilfredo na Emile Durkheim na baadaye iliendelezwa na mwana anthropolojia Radcliffe Brown na Malinowski Malinowski (Wallance na Wolf, 1980). Nadharia ya Uamilifu huzingatia kuwa fasihi simulizi inatenda kazi kutokana na mfumo uliyopo katika jamii. Aidha, Nadharia hii huchunguza dhima za kazi za fasihi katika jamii. Kwa kuwa makala hii imelenga kuchunguza mbinu, dhima na athari za kumuanika nje mfiwa katika utendaji wa utani wa Wahehe, nadharia hii imetusaidia kwenye uchambuzi wetu, hasa katika kipengele cha dhima na athari za kumuanika nje mfiwa. Kwa ujumla, Nadharia ya Utendaji imetusaidia kujuu namna utani unavyotendeka baada ya mfiwa kuanikwa nje na Nadharia ya Uamilifu imetusaidia kujuu dhima na athari za mfiwa kuanikwa nje katika jamii ya Wahehe. Baada ya utangulizi huu, sehemu inayofuata inaelezea mbinu, dhima na athari za kumuanika nje mfiwa katika utendaji wa utani wa Wahehe. Sehemu hii itafuatiwa na uchambuzi wa mbinu za kiutendaji wa utani wakati wa kumuanika nje mfiwa, dhima, athari zake na mwisho hitimisho.

Utendaji wa Utani katika Jamii ya Wahehe

Sehemu hii inaeleza utendaji wa utani tuliyoubainisha katika jamii ya wahehe. Utendaji ni uti wa mgongo wa fasihi simulizi kwani ndio unaoitofautisha fasihi simulizi na fasihi andishi (taz Bauman 1984; Thiong'o 2007; Finnegan 2012 na Mulokozi 2017). Muluka (1999) anafafanua utendaji kuwa ni uwasilishaji wa hadithi au ngano unaofanywa na msanii kwa hadhira kwa kutumia mdomo na kuambatana na matendo ya viungo mbalimbali vya mwili na ishara ya uso. Hivyo, kwa kuwa utendaji ni uti wa mgongo wa fasihi simulizi, ni dhahiri kuwa utendaji hauepukiki katika utani unaofanyika katika jamii ya Wahehe pamoja na kwamba unaweza kutofautiana. Okpewho (1992) anaeleza kuwa utendaji unatofautiana kutoka jamii moja hadi jamii nyingine kwa sababu ya umri wa fanani, umri wa hadhira, nguvu ya fanana kwa sababu baadhi ya vipera kama vile majigambo vinahitaji fanani awe na nguvu, tukio husika mfano utendaji katika msiba hauwezi kufanana na sherehe, mandhari au jukwaa la kutendea, vifaa vinavyotumika na fanani katika utendaji kama vile maleba na mkuki, na idadi ya fanani.

Utendaji katika jamii ya Wahehe hufanyika iwapo kuna mtani au watani (fanani) pamoja na hadhira katika eneo la tukio. Watani wa jamii ya Wahehe ni pamoja na Wasukuma, Wangoni na Wazaramo. Mulokozi (1996, 2017) anaeleza kuwa utendaji hujumuisha fanani na hadhira kukutana pamoja. Hadhira hupokea ujumbe na pia kushiriki katika kufanikisha utendaji kwa kuitikia, kupiga kelele, vigegele, kutumia ala za muziki kama filimbi, kupiga ngoma na kuonesha ishara za usoni. Mulokozi anaendelea kuelezea kuwa uwanja wa kutendea ni mahali au jukwaa la utendaji au sehemu ambapo tukio la utendaji hufanyika na muktadha hufafanua mazingira ya tukio husika. Katika maelezo haya, Mulokozi (2017) anabainisha vipengele nane ambavyo ni fanani, hadhira, fani inayotendwa, maudhui yanayoleezwa, tukio, kusudio la kisanaa, mahali na wakati. Mambo hayo nane yamekuwa msaada mkubwa kwa utafiti huu katika kujadili mbinu ya kumuanika nje mfiwa na athari zake katika utendaji wa utani wa Wahehe. Mulokozi anaendelea kufafanua nyenzo za utendaji ambazo ni kuitikia, kupiga kelele, vigegele na kutumia ala za muziki kama filimbi, kupiga ngoma na kuonyesha ishara za usoni. Kutokana na umuhimu wa utendaji katika fasihi simulizi makala yetu imeelezea namna utani unavyotendeka katika jamii ya Wahehe kupitia mbinu ya kumuanika nje mfiwa.

Mbinu ya ‘Kumuanika Nje Mfiwa’

Mbinu ni kipengele kimojawapo cha mtindo katika kazi ya fasihi, ambapo kuna mbinu za utunzi na mbinu za utendaji. TUKI (2014) wanafasili mbinu kama njia zenye hila na ujanja za kufanyia jambo.

Mbinu za utunzi hujumuisha vipengele vya matumizi ya lughu, mbinu za kiuandishi na matumizi ya picha (Haji, 2015). Hivyo, mbinu ni ubunifu wa mtunzi au mwandishi katika kazi ya fasihi. Utani kama kipera cha fasihi simulizi pia kina mbinu zake za kiutunzi na kiutendaji zinazotumika. Utafiti huu umechambua utendaji wa utani wa jamii ya Wahehe wakati mfiwa anapoanikwa nje kama mbinu mojawapo ya utani. Uanikaji nje wa mfiwa kama mbinu mojawapo ya utendaji wa utani katika jamii ya Wahehe husukwa kwa ufundu kiasi cha kumfanya mfiwa na mtani kuelewana na kuruhusu suala la utani kuendelea.

Katika jamii ya Wahehe unapotokea msiba unaohusisha watani (Wangoni, Wasukuma, Wazaramo nk) mfiwa huanikwa nje kwa lengo la kutaniana. Kwa mfano, mtarifitishu alishuhudia msiba uliyotokea Wilayani Kilolo mkoani Iringa, ambapo jamii ya Wahehe ilipata msiba na Mngoni (mtani) ambaye alikuwepo katika mazingira hayo kitu kilichosababisha utani kuibuka katika msiba huo. Utendaji wa utani katika msiba huo ulijidhihirisha pale mtani alipokuwa anamtoa mfiwa nje kwa lengo la kwenda kumuanika. Aidha, katika tukio hilo utani ulikuwa umesukwa kwa ubunifu mkubwa. Utendaji wa utani katika jamii ya Wahehe msibani huwa na msoko kadhaa wa matukio, ambapo utokeaji wa tukio moja husababisha utokeaji wa tukio jingine. Mjengo wa matukio huo unajidhihirisha katika mkururo ufuataao.

Mtani kuanza na Kicheko

Utafiti huu umebaini kuwa pindi mtani anapowasili msibani ambako ni kwa mtani wake huanza na kicheko badala ya kilio kama wanavyofanya watu/wafiwa wengine. Kicheko hiki kwa watu ambaao ni jamii zinazohusika huwa ni kielelezo kuwa mtani ameshafika msibani. Akishacheka akiwa nje huungia ndani ambako kwa kawaida huwa na wafiwa wa aina mbalimbali na waombolezaji ambako huendeleza utani wa kicheko na maneno ya kejeli kama vile leo "*mtani kapatikana mpaka analia*". Utani huu hulusisha mfiwa mkuu mathalani, mke akifiwa na mume au mtoto na hata mume akifiwa na mke au mtoto. Baadaye mtani huenda moja kwa moja kwa mfiwa na kuanza kumchekeea wakati huo mfiwa analia. Mtani huendelea kucheka na kumtolea mfiwa maneno ya dhihaka. Mtarifitishu alipomhoji mtani kuwa kwa nini anacheke badala ya kulia msibani ina maana amefurahia kifo kutokea? Mtani alijibu kuwa hiyo ni kawaida ya mila na desturi kwa jamii yoyote anayofanyiana utani. Aliendelea kusema, siyo kama anafurahia bali ana uchungu kama wafiwa wengine lakini ni lazima afanye vile kwa sababu yule ni mtani na hana budi kutaniwa kama ilivyo desturi yao. Aidha, kicheko husababisha mtani kuwambia wafiwa wanyamaze kulia, wanampigia kelele kwani wao sio watu wa kwanza kufiwa.

Kuwaamuru Wafiwa Kunyamaza

Katika utendaji wa utani katika jamii ya Wahehe, msoko unaendelea pale ambapo mtani anawambia wafiwa wanyamaze kulia kwani wanampigia kelele kwa kuwa wao sio watu wa kwanza kufiwa. Utafiti wetu umebaini kuwa mara baada ya mtani kucheka msibani humtaka mfiwa anyamaze kulia kwa kigezo cha kuwa anampigia kelele. Kupiga kelele kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu niIwapo mfiwa ataendelea kulia mtani huchukulia kama ni dharau na kuamua kutoka naye nje ya chumba walichotenga kwa ajili ya msiba na kwenda kumuanika nje (juani). Utokaji wa mfiwa nje huwa ni wa lazima na mtani huweza kutumia hata nguvu. Endapo atajitokeza mtu na kuanza kumuongelea tofauti mtani kama vile mtani kutokuona kama mfiwa ana uchungu basi mtani humchukua na huyo anayeongea na kuwaanika wote juani. Kitendo cha kutolewa nje mfiwa huongeza uchungu zaidi hali inayopelekea kulia sana. Mfiwa anapolia sana mtani hufurahia kwani huamini kuwa atapata fedha nyingi kwani watu waliyopo msibani watamuonea huruma mfiwa na kuamua kumkomboa kwa kutoa fedha nyingi ili mfiwa arudi ndani. Mtarifitishu alimuhoji mtarifitishu kuwa utani wao hutokea mfiwa anapoamuliwa kwenda nje pekee? Mtarifitishu alieleza kuwa hata bila ya kuamuriwa bado mfiwa hutakiwa kwenda nje kuanikwa kama ilivyo kawaida yao wanapokutana kwenye matukio ya msiba.

Mtani Kukusanya Fedha kutoka kwa Waombolezaji ili Kumkomboa Mfiwa

Baada ya mtani kumuanika mfiwa na watu wa jirani (hasa ndugu) wa mfiwa nje, suala la ukusanyaji wa fedha kutoka kwa waombolezaji hufuatia. Ukusanyaji wa fedha kwa waombolezaji huenda sambamba na maneno ya kejeli na dharau kwa wafiwa na waombolezaji. Mathalani, mtani alisikika akisema "*Hahaaaaaa!!!!!! Wahehe huwa mnajifanya wajanja sana sasa inakuwaje mpaka sasa nimepata shilingi elfu kumi tu*". Maneno haya yanapotolewa na mtani huwa na lengo la kuwashamasisha watu kutoa fedha zaidi ili kuweza kufikia kiwango anachokihitaji. Mfiwa pamoja na ndugu zake wanaweza kukaa juani zaidi ya saa moja, kama hali ya utoaji wa fedha ya kumkomboa itakuwa haimridhishi mtani. Hali hii hufanya kila mtu aliyejuwa msibani kujitahidi kutoa fedha ya kiwango chochote ili kumuondoa mfiwa juani. Katika ukusanyaji wa fedha hii mtani hukusanya fedha ya noti na chenji.

Mtani Kugoma Kurudisha Chenji

Katika jamii ya Wahehe utani huendelea baada ya mfiwa kurudishwa ndani. Katika hatua hii utani huibuka kati ya mkusanyaji wa fedha na mtoaji wa fedha kubwa kama shilingi elfu tano (5000) na elfu kumi (10000). Mtafiti alipomhoji mtafitiwa kwa nini watu waliyotoa fedha kubwa hakuwarudishiwa chenji zao alijibu kuwa "*Wahehe wanajifanya wana fedha kuliko Wangoni na ndiyo maana wamekuja na noti kubwa*" hivyo, chenji zao atawapa atakapopenda yeye na siyo wanavyotaka wao. Baada ya mtani kuwa mgumu kurudisha chenji za baadhi ya waombolezaji mtafiti alishuhudia waombolezaji wengine waliosikika wakisema yeye (mtoaji wa fedha ya shilingi 5000) mgeni na Mngoni? Hakupaswa kutoa fedha yote kwake angetafuta chenji kwa watu wengine kwani atamsumbuwa sana kumpa chenji na atampa muda atakaotaka yeye. Hata hivyo, baadaye mtani (Mngoni) alishuhudiwa akirudisha chenji hadharani na kumuonya mtoaji kuwa siku nyingine asirudie tena kwani 'kilichoenda kwa mganga huwa hakirudi'. Aidha, mngoni alifafanua kuwa amerudisha fedha ile hadharani ili jamii isije ikafikiri mtani aliondoka na chenji za watu. Kwani hata kama anakusanya pesa na kufanya vicheko na kebehi bado ule ni utani tu ambaa huwa na lengo la kupunguza uchungu kwa wafiwa na kuwafanya wasiisisikie upweke.

Mtani Kupanga na Kufanya Matumizi ya Fedha za utani

Baada ya kukusanya fedha msuko wa utani huendelea pale mtani anapoamua kwenda kununua kanga au kitenge kwa ajili ya kuja kumvalisha mfiwa. Mtafiti alishuhudia mtani akienda kununua kanga ya kumvalisha mfiwa baada ya kukusanya pesa kutoka kwa waombolezaji. Mtani alikwenda kununua doti ya kanga nzuri kwa ajili ya mfiwa na nguo hii alimvalisha mfiwa baada ya maziko. Baada ya kununua kanga mtani alichukua kiasi kidogo cha fedha na kusema naye anakwenda kunywa soda kwani hawezu kufanya kazi ya kuwakiwa na jua bure. Aidha aliongeza kuwa, siku hizi hakuna kitu cha bure na kwamba kila kitu ni pesa hivyo naye aliquwa kazini. Hata hivyo, baada ya kununua kanga na mtani kuchukua kiasi kidogo cha fedha kiasi kilichobaki alikikabidhi kwa mfiwa. Sambamba na hili wakati wa matangazo na taarifa ya fedha iliyopatikana kwenye msiba kiasi cha fedha kilichokusanywa na Mngoni (ambaye ndiyo mtani) kilitangazwa makaburini. Kitendo hiki cha kutangaza fedha iliyokusanywa makaburini kinaonesha suala la uwazi na kuwepo kwa mwendelezo wa kaida ya kufanyiana utani katika jamii hizi. Na hii inatupa mwangaza wa kujua kuwa haya mambo yapo katika jamii zetu na watu wanafanyiana kwa malengo mbambali kama yanavyofafanuliwa hapa chini kwenye dhima na athari za kumuanika mfiwa nje.

Dhima na Athari za Kumuanika Mfiwa Nje wakati wa Utendaji wa Utani

Utafiti ulibaini tija na madhara ya utendaji utani katika jamii ya Wahehe wakati wa kumuanika mfiwa nje. Hata hivyo, kiasi cha madhara ni kidogo kikilinganishwa na tija. Baadhi ya dhima za kumuanika nje mfiwa wakati wa utendaji wa utani ni pamoja na:

Kujenga Umoja na Ushirikiano

Makala imebaini kuwa mbinu ya kumuanika nje mfiwa wakati wa utendaji wa utani katika jamii ya Wahehe imesaidia sana katika kujenga umoja na ushirikiano. Utendaji wa utani huu ambao hutumia lugha ya kejeli na dhihaka wakati wa msiba na hasa mfiwa anapoanikwa nje hutumika katika kuwaunganisha watu badala ya kuwatenganisha watani hawa moja kwa moja. Mathalani, kutokana na maelezo ya mtani (Mngoni) aliyejohiana na mtafiti anasema utani kati ya jamii ya Wahehe na Wangoni kwenye misiba upo tena kwa kiwango kikubwa japo siyo sawa na zamani ambapo utani ulikuwa wa vitendo na maneno. Hata hivyo, anaendelea kusema kuwa tangu awali watani hawa walikuwa wakitaniana katika shughuli kama ugonjwa, harusi na misiba. Aidha, katika msiba mtani akifiwa (ambaye anaweza kuwa Mhehe au Mngoni) hushiriki tukio lote la msiba kwa njia ya utani na hii huwasaidia kuwaweka pamoja hata kama mtani anaweza kuwa peke yake katika eneo husika lakini uwepo wa khabila ambalo wanafanyiana utani husaidia kuwaweka pamoja na hivyo kumuondolea upweke mhusika kwani watu wengi hushiriki katika tukio lake. Hivyo, utani si ugomvi bali hutumika kama mbinu ya kujenga umoja na ushirikiano baina yao. Hali hii ya umoja na mshikamano pia mtafiti alishuhudia msibani pindi jamii ya Wahehe walipopata msiba na mtani (mngoni) alipofika msibani na kuendeleza utani. Hali ilikua tofauti na alivyokuwa anafikiri mtafiti kwani jamii zote mbili zilijitokeza msibani na kushirikiana katika masuala ya mapishi, kuosha maiti, kuchimba kaburi na kuzika japo matukio yote yalitendeka kwa kuongozwa na utani.

Kupunguza Majonzi kwa Wafiwa

Utendaji wa utani katika jamii ya Wahehe kuititia mbinu ya kumuanika nje mfiwa husaidia kupunguza majonzi kwa wafiwa. Mathalani, mtani anapoingia eneo la msiba na kuanza kucheka, hali hii huifanya hadhira iliyopo ishangae kwani huwa kinyume na taratibu za mila na desturi za jamii nyingi, ambapo badala ya kulia mtani hucheka. Hali hii inapojitokeza watu wenye uzoefu na masuala ya utani hubaini moja kwa moja kuwa mtani yupo eneo la tukio na hivyo hutarajia maneno, kejeli na dhihaka mbalimbali toka kwa mtani. Mathalani, mtafiti alishuhudia mtani akicheka na kuwambia wafiwa nyamazeni kulia na kupiga kelele kwani nyie ndiyo watu wa kwanza kufiwa? Kwani hata kama mkilia mpaka mle kamasi huyo mtu atarudi? Maneno haya ambayo huambatana na vitendo kama kutikisa mwili, kupiga makofi, kubetua midomo, kupiga vigelegele na kurukaruka hufanya hadhira iliyopo ishangae na wakati mwininge kucheka. Mtafiti alipomhoji mtafitiwa (fanani) alisema haya yote hufanyika kwa lengo la kupunguza machungu na huzuni kwa mfiwa. Kwani bila maneno haya ya utani mfiwa anaweza kulia tu muda wote hali inayoweza kusababisha kuumwa na kuchoka zaidi kimwili. Hivyo, utani unaotendwa kuititia maneno ya kejeli na dhihaka huwaburudisha wafiwa na waombolezaji walijopo kwenye tukio. Aidha, mhojiwa alisisitiza kuwa yeze anapofanya utani siyo kama hana uchungu lakini hulazimika kufanya hivyo ili kuendeleza kipera hiki cha utani na kumuondolea machungu mfiwa na waombolezaji wengine.

Kulinda na Kuendeleza Amali hii Muhimu katika Jamii

Utani ni kipera cha fasihi simulizi kinachojibainisha katika jamii nyingi za Kiafrika. Pia, utani ni kiunganishi cha mila na desturi za Waafrika. Kutokana na umuhimu huu, amali hii imekuwa ikilindwa na kuendelezwa katika jamii ya Wahehe kuititia matukio kama misiba, sherehe pamoja na shughuli za uzalishaji mali. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha mbinu ya kumuanika nje mfiwa, huendeleza kipengele hiki cha utani kuititia utendaji. Mathalani, mfiwa anapoanikwa nje watu ambao hawajui masuala ya utani huweza kubaini kuwa jamii zetu bado zinatunza na kuendeleza mila na desturi hizi ambazo zilikuwepo tangu enzi za mababu zetu. Hali inayosababisha hata jamii ya sasa kuendeleza utani kwa kutumia mbinu za kitekinolojia kama facebook, twitter, whatsapp na mitandao mingine ya kijamii.

Athari ya Kumuanika Mfiwa Nje wakati wa Utendaji wa Utani

Licha ya dhima za kumuanika nje mfiwa, pia kuititia data iliyokusanywa imeonekana kuwa zipo athari zake. Sehemu inayofuata inaonesha athari hizo.

Kuzua Mshangao na Taharuki kwa Waombolezaji

Utafiti umebaini kuwa mfiwa anapoanikwa nje kuna baadhi ya watu ambao huwa hawana usuli wa utamaduni huo upata mshangao na taharuki. Watu hao ambao huwa wanakuja kwenye msiba kwaajili ya kumfariji mfiwa hushangaa na wakati mwingine hukasirika kwa matendo na maneno anayoyafanya mtani.

Mtani Kuchukiwa

Kumwanika mfiwa nje pia kuna athari kwa mtani kutokana na utani anaoufanya. Kwa mfano, kutokana na maelezo ya mtani (Mngoni), alimwambia mtafiti changamoto wanazokutana nazo na watu wasiyojua maana ya utani ni pamoja na kulaumiwa, kutukanwa, na wakati mwingine kutaka kupigwa. Hata hivyo, mtafitiwa aliendelea kusema kuwa watu aina hii wakijitokeza kutaka kufanya vurugu huonywa na wazee wa jamii husika kwa kuwafafanulia kuwa huu ni utani tu wenye lengo la kupunguza huzuni na machungu kwa wafiwa na si vinginevyo.

Hitimisho

Makala hii imechunguza mbinu, dhima na athari za kumuanija nje mfiwa katika utendaji wa utani wa Wahehe. Imebainika kuwa kuna msuko unaofuatwa wakati wa kumuanika nje mfiwa. Msuko huo huhusisha mambo kama vile; mtani kuanza kwa kicheko, kuwaamuru wafiwa wanyamaze kwani wao sio watu wa kwanza kufiwa na atakayekaidi maelezo yake atamtoa kwa nguvu nje na kumuanika juani, kukusanya fedha kutoka kwa kila mta aliyekwenda msibani kwa ajili ya kumkomboa mfiwa na mwisho fedha iliyokusanywa hutumika kununua kanga/kitenge cha mfiwa na kiasi kilichobaki hupewa mfiwa na kiasi kidogo huchukua mtani. Kupitia hatua hizi utani umekuwa ukitendeka na kuendelezwa katika jamii ya Wahehe. Aidha, makala imebaini kuwa utani unaotendeka kwa kutumia mbinu ya kumuanika nje mfiwa huwa na dhima na athari pia. Baadhi ya dhima hizo ni pamoja na kujenga umoja na ushirikiano, kupunguza majonzi kwa wafiwa pamoja na kuendeleza amali hii muhimu mionganoni mwa wana jamii. Athari zilizobainishwa ni pamoja na kuzua mshangao na taharuki pamoja na chuki mionganoni mwa waombolezaji na mtani. Hata hivyo, athari hasi ni chache kuliko dhima zinazopatikana katika utani ambazo zinaendeleza fasihi simulizi pamoja na ushirikiano baina ya jamii na jamii. Katika fasihi simulizi utendaji ndiyo sifa pekee na ya msingi inayotofautisha fasihi simulizi na fasihi andishi (Thiong'o, 2007, Finnegan, 2012 na Mulokozi 2017).

Marejeleo

- Bauman, R. (2011). *Exploration in the Ethnography of Communication*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Finnegan, R. (2012). *Oral Literature in Africa*. Cambridge: Open Book Publishers.
- Foley, J. (1995) *The Singer of the Tales in Performance*. Bloomington: Indiana University Press.
- King'ei, G. K na Kisovi, C. N. M. (2005). *Misingi ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria.
- Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Fasihi Vyuoni na Vjuo Vikuu*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.
- Msokile, M. (1992). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. East African Education Publishers.
- Okpewho, I. (1992). *African Oral Literature: Background, Character and Continuity*. Bloomington: Indiana University Press.
- Schechner, R. (2013). *Performance Studies: An Introduction*. New York: Routledge.
- TUKI (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- Thiong'o, N. (2007). "Notes Towards a Performance Theory of Orature." Perfomarnc Research. 12 (3): 4-7
- Wallance, R. A na Wolf, A. (1980). *Contemporary Sociological Theory*. New York: Prentice Hall Publishers.